



Alhamisi Machi 21, 2019

Tanzani 500/- Kenya 50/-



MAHABA YA

**MAVOKO
ATAMANI
KUFA**

**LULU,
PREZZO**





MAHABA YA AMBER LULU, PREZZO YATAMATIKA

Na Mary Kadoke

Na Mary Kadoke
PAMOJA na kujishuka kote, hatimaye
mkali wa ngoma ya Jini Kisirani Amber
Lulu amebwaga manyanga kwa mpenzi
wake Mkenya Prezzo.

Akizungumza na Alasiri Online Amber
amesema amekuja kugundua ali-
poteza muda kwa mpenzi wake huyo
aliyedhani atampenda kama ampen-
davyo.

"Hakukuwa na mapenzi, ni full ku-
umizwa nilipoteza muda wangu mwini-
gi sana, wakati mapenzi hayakuwepo
hata chembe," amesema.

Awali Amber alijishusha na kuomba
msamaha baby wake baada ya video
yake akiwa na muimbaji Nuh Mziwan-
da faragha wakipeana mabusu kuvuja
mitandaoni.

Baada ya skendo hiyo aliamua kumu-
omba msamaha Prezzo na safari yao ya
mapenzi kurejea upya, sasa wamefika
tamati na kila mmoja amechukua ham-
sini zake.

Eti mwanamke atavuruga bendi

Na Anaeli Mbise

UONGOZI wa bendi ya Inafrika umesema unaogopa
kumwajiri mwimbaji wa kike ili kuweka hali ya utu-
livu kwa wanamuziki wake amba wote ni wanaume.

Akizungumza na Alasiri Online, mkurugezi wa ben-
di hiyo Roy Figweiredo, amesema kuwa na mwimbaji
wa kike ni sawa na kukaribisha chuki inayotokana na
wivu mionganini mwa wanamuziki.

"Syo kwamba hatutaki mwimbaji wa kike, ila tu-
naogopa vurugu kwa sababu baadhi ya wanamuziki
wa kiume wakiona mwanamke kila mmoja anatumia
nguvu yake kujisogeza na kusababisha vurugu,"



amesema Figweiredo.

Aidha amesema kuwa ili muziki wa dansi uzidi ku-
fanya vizuri wanamuziki kupendana katika kazi.

Bendi hiyo imewahi ku-
tamba na nyimbo kama

Yalla Yallah, Indege na
Julie.

 HABARI KITAIFA

MASTER J

AMZIMIA HARMAONIZE


Na Anaeli Mbise

PRODUCER mkongwe wa muziki wa kizazi kipywa Master J amesema kuwa anapenda kusikiliza nyimbo za Harmonize kutohana na ujuzi alionao msanii huyo.

Akizungumza na Alasiri Online, Master J amesema kuwa mwanamuziki huyo ni mbishi na hakubali kushindwa katika game ya muziki na nyimbo zake ni nzuri.

"Harmonize nampenda na namkubali

sana alivyokuja BSS alikuwa bado hajakomaa ila dogo ni mbishi na anajua namna ya kutega mashabiki kwa ngoma zake hizo," amesema Master J.

Kadhalika Producer huyo amesisistiza kuwa ili wanamuziki wa kizazi kipywa wazidi kupaa kitaifa na kimataifa hawa-

na budi kutunga mashairi ya kuelimisha jammii na siyo tu kuimba mapenzi.

Akizungumzia namna alivyomwagisha sifa hizo, Harmonize amesema kuwa amefurahishwa na kitendo hicho kwa sababu producer huyo anajua mwana-muziki bora na ambaye siyo bora.

MAVOKO ATAMANI KUFA

Na Mary Kadoke

MUIMBAJI nguli kutoka tasnia ya Bongo Fleva, Rich Mavoko, amesema siku zake za kuishi hapa duniani zinahesabika.

Amesema hayo kupitia ukurasa wake wa Instagram @richmavoko pasipo kufafanua kilichomsibu mpaka kufikia kufunguka maneno hayo.

"Ni siku ya mwisho ya maisha yangu yalibaki," aliandika.

Hata hivyo baada ya Alasiri Online kumsaka kwa hali na mali ili aeleze kuhusu maono yake, juhudzi hazikuzaa matunda.

Aidha baada ya kuandika ujumbe wake huo, ni kama vile alifuingua uwanja wa maoni mbalimbali kutoka kwa mashabiki zake wakijuliza maswali yaliyokosa majibu kupitia ukurasa huo.

"kafulia Mavoko," aliandika loniwiz_tz.

"Ngoma mpya inakuja ya Mess wa Bongo@richmavoko," aliandika brightonmagakila.





Temba apika Washa

Na Anaeli Mbise

MSANII wa Hip hop nchini Mheshimiwa Temba amesema kuwa anatarajia kutoa ngoma mpya inayokwenda kwa jina la

Washa.

Akizungumza na Alasiri Online, mwanamuziki huyo amesema kuwa baada ya kimya cha muda mrefu anatarajia mwishoni wa Machi kutoa ngoma

hiyo ambayo itakuwa ni ya kwanza tangu mwaka huu uanze.

Akizungumzia maudhui yanayopatikana katika ngoma hiyo amesema kuwa unazungumzia namna ambavyo mtu anatakiwa kufanya kazi kwa bidii kama ambavyo moto huwa

unawaka ukiwasha na kiberiti.

“Ni ngoma ambayo itakuwa ina mambo ya kupiga job kwa kasi na kupiga dili za mahela tu ni kusaka chapaa hadi kisomeke ni washaka kama unawasha moto vile,” amesema Temba.

Mwanamuziki huyo baada ya kutamba na ngoma kama vile Nipe Mimi, Nawachanganya, Enzi Zetu, Amekoma pamoja na Kiulaini, huku akisema kuwa ngoma hiyo mpya itatengenezwa na studio za Mr. Laiza.

Young Killer aamua magumu



Na Mary Kadoke

HUKU baadhi ya wasanii wa Bongo Fleva wakihangaika kupata menejimenti itakayosimamia kazi zao, mfokaji Young Killer

amesema ye ye mwenyewe anajitosheleza.

Amesema hayo alipofanya mazungumzo na Alasiri Online akisisitiza kuwa hana mpango huo kwa sasa.

“Kama ni maamuzi ya kuwa na menejimenti mpaka sasa ningekuwa nayo kwani

ni wengi wanaotaka kufanya hivyo,” amesema.

“Menejimenti ni mimi mwenyewe,” amelizia.

Miongoni mwa wasanii wanaohaha kila uchao mitandaoni kusaka menejimenti ni

muimbaji Sr Fey ambaye mara nyingi hutumia ukurasa wake wa Instagram fey_tanzania kutoa maombi yake.

Mfokaji Young aliwahi kutamba na kibao chake cha Mwanza Mwanza kilichomtambulisha kwa kiasi kikubwa.